# MSITU

Ruhusa ya kutumia nyaraka hii kwa kupeyana bure kupitiya maandishi na njia nyengine imepewanywa, ile tuu mongabay.com ipewe sifa ya mwanzishi.

Mongabay.com inalenga kuinua uvutio wa wanyama na mbuga zao ikijulisha juu ya mambo ya mazingira.  Kama haijatajwa mambo yote kwa hii tovuti imeandikwa na Rhett Butler.

**Misitu ya mvua ni nini?**

--------------------------------------------------------------------------------

Misitu ya mvua ya eneo ya joto ni misitu ambaye ina miti mirefu, hewa ya joto na mvua nyingi.  Kwa misitu ya mvua nyingine inanyesha zaidi ya inchi moja kila siku!

Misitu ya vua inapatikana Afrika, Asia, Australia, Amerika ya kati na ya kusini.  Msitu wa mvua ambaye ni kubwa zaidi ni msitu wa mvua wa Amazon.

**Msitu ya mvua inapatikana wapi?**

--------------------------------------------------------------------------------

Misitu ya mvua inapatikana kwa eneo ya jua katikati ya eneo ya Capricorn na eneo ya Cancer Kwa hii eneo, jua inakuwanga joto na inang'ara kwa kiasi sawa kila siku ya mwaka nainafanya hewa ikuwe joto na ya usawa.

Nchi nyingi zina msitu wa mvua   Nchi ambacho zina kiwango kubwa zaidi ya msitu wa mvua ni:

1  Brazil
2  Jamhuri ya Demokrasia ya Congo
3  Peru
4  Indonesia
5  Colombia
6  Papua New Guinea
7  Venezuela
8  Bolivia
9  Mexico
10 Surinam

**MSITU WA MVUA NI NINI?**

--------------------------------------------------------------------------------

Kila msitu wa mvua ni tofauti lakini kuna mambo fulani ambaye inapatikana kwa kila msitu ya mvua.

+ Mahali Misitu ya mvua inapatikana kwa eneo ya jua "tropiki"
+ Mvua: misitu ya mvua inapata angalau inchi 80 za mvua kila mwaka
+ Mwavuli:  misitu ya mvua ina mwavuli ambaye ni safu ya matawi na majani inayotengezwa na miti ya msitu wa mvua inayopatana karibu.  Karibu mimea na wanyama wote wa msitu wa mvua wanaishi kwa mwavuli. Mwavuli inaweza kuwa futi 100 kutoka chini.
+ Mazingira tofauti: misitu ya mvua ina kiwango kikubwa cha utofauti wa biolojia au mazingira tofuati  Biodiversity au utafauti wa biolojia ni jina ya viumbo vyote ambacho ziko hai – mimea, wanyama na uyoga – inayopatikana kwa mazingira. Wanasayansi wanaamini kwamba karibu nusu ya mimea na wanyama inayopatikana kwa ardhi ya dunia inaishi kwa misitu ya mvua

+ Hali ya utengemeano kati ya viumbo: Viumbo ndani ya msitu wa mvua mara nyingi ufanya kazi pamoja. Uhusiano wa utengemeano ni uhusiano ambayo viumbo viwili zinafaidika kwa kusaidiana. Kwa mfano mimea nyingine zinatengezea wadudu miundo ya mazingira na sukari. Hawa wadudu nawo wanalinda mimea hii kutoka kwa wadudu wengine wangeotaka kukula majani yao.

**MWAVULI NI NINI?**
--------------------------------------------------------------------------------

Kwa msitu wa mvua karibu mimea na wanyama wote hawapatikani kwa sakafu ya msitu mbali wanapatikana dunia ya majani inayojulikana kama mwavuli. Mwavuli ambayo inaweza kuwa futi 100 juu ya ardhi inatengezwa na mchanganyiko wa matawi na majani ya miti ya msitu wa mvua. Wasayansi wanakadiria kwamba asilimia 70-90 ya maisha ya msitu wa mvua inapatikana kwa miti, na ifanya hii iwe mazingira kubwa zaidi ya mimea na wanyama. Wanyama wengi wanayojulikana kama tumbili, chura, vijusi, ndege, nyoka na paka ndogo zinapatikana kwa mwavuli.

Mazingira ya mwavuli ni tofauti sana na mazingira ya sakafu ya msitu Mchana, mwavuli inakuwanga imekauka nainakuwa na joto kushinda sehemu zingine za msitu na mimea na wanyama wanayoishi huko wamezoeya hii maisha ya miti. Kwa mfano kwa sababu kiwango ya majani kwa mwavuli inaifanya ngumu kuona mbele ya futi chache, wanyama wengi wa mwavuli wanatengemea mwito wa sauti kubwa au nyimbo kwa uwasiliano. Vipengo kati ya miti inaimaanisha kwamba wanyama wengine wa mwavuli wanaruka au wanaenea juu ya miti.

Wanasayansi kwa muda mrefu wamekuwa wakitaka kuchunguza mwavuli lakini kwa sababu ya urefu wa miti ya misitu ya mvua utafiti mpaka hivi karibuni umekuwa shida. Siku hizi kuna mahali maalum zinayo na daraja za kamba, ngazi na minara kusaidia wanasayansi kuzumbua siri za mwavuli.

Mwavuli ni moja tu wa safu za wima kadhaa ndani ya msitu wa mvua. Anghalia diagram upande wa ushoto kuona mipangilio nyengine ( overstory, understory, mpangilio wa kichaka na sakafu ya msitu).

**SAKAFU YA MSITU WA MVUA**
--------------------------------------------------------------------------------

Majani ya mwavuli inafanya safu ya ardhi ya msitu wa mvua mara mingi uwe mahali ya giza na unyevu. Lakina licha ya mvuli yake daima, sakafu ya msitu wa mvua ni sehemu muhimu ya mazingira ya msitu.

Sakafu ya msitu ndipo uozaji unatokea. Uozaji ni njia ambaye viumbo kama uyoga na zingine ndogo zinazemea mimea na wanyama wasiyo hai na kurejesha vifaa na malisho muhimu.

Wengi wa waanyama kubwa zaidi wa msitu wa mvua wanapatikana kwa sakafu ya msitu. Wengine ni kama ndovu, tapir na jaguar.

**KWA NINI MISITU YA MVUA INA AINA NYINGI YA MIMEA NA WANYAMA?**
--------------------------------------------------------------------------------

Misitu ya mvua ya tropiki inalisha aina kubwa zaidi ya viumbo venye hai duniani. Licha ya kuchukuwa chini ya asilimia 2 ya ukumbwa ya ardhi ya dunia misitu ya mvua iko na juu ya asilimia 50 ya mimea na wanyama duniani. Hapa kuna mfano wa utajiri wa misitu ya mvua:
+ misitu ya mvua ina aina ya 170,000 ya mimea 250,000 ya dunia ambayo inajulikana

+ Marekani ina aina ya chura 81 naye Madagascar ambaye ni ndogo kushinda Texas ina aina 300.
+ Europa ina aina ya vipepeo 321 nayo mbuga wa msitu wa mvua wa Peru (Mbuga wa Taifa wa Manu) una aina 1300.
Misitu ya mvua ina mimea na wanyama wengi kwa sababu zifuatayo:
+ Hewa: kwa sababu misitu ya mvua inapatikana kwa eneo ya tropiki ina pata jua nyingi. Hii jua inabadilishwa kuwa kawi na mimea ikitumia njia ya usanidinuru. Kwa sababu kuna jua nyingi hii inaimaanisha kuwa kawi nyingi kwa msitu wa mvua. Hii kawi inawekwa kwa mimea inayokulwa na wanyama. Kwa sababu kuna chakula nyingi kuna aina nyingi ya mimea na wanyama.
+ Mwavuli:  hali ya mwavuli inaimaanisha kuna sehemu nyingi ya mimea kukuwa na wanyama kuishi. Mwavuli inapeyana njia mpya ya chakula, malazo, na mahali ya kujifisha na inapeyana pahali pengine pa viumbo mbali mbali kuathiriana.   Kwa mfano kuna mimea kwa jina bromeliads ambayo inahifadhi maji kwa majani yake. Wanyama kama chura wanatumia mifuko wa maji kwa kuwinda na kutaga mayai.

**MAMALIA ZA MSITU WA MVUA**
--------------------------------------------------------------------------------

Msitu ya mvua ya tropiki ni makao ya aina nyingi ya mamalia. Chini kuna maelezo ya mamalia wachache wa msitu wa mvua.

MAMALIA ZA HALI YA JUU
Gray Titi ya Bolivia
Tumbili ya Dusky Titi
Ebony Langur
Golden Lion Tamarin
Sokwe
Lemurs
Macaque wenye Mkia Mrefu
Macaque
Orangutan
Tumbili ya Proboscis
Tumbili ya Squirrel
Wied’s Tufted-Eared Marmoset
Tumbili ya Woolly
PAKA
Jaguar
Ocelot

ZINGINE
Nyati ya Afrika ya Msitu
Nyati ya Afrika ya Msitu
Agouti
Babirusa
Popo
Nguruwe yenye Ndevu
Capybara
Coatimundi
Ndovu
Giant Anteater
Otter Nene ya Mto
Tapir ya Malaya
Okapi
Sloth
Kifaru ya Sumatra
Tapir

Nguruwe Mwitu

**NDEGE ZA MSITU WA MVUA**

---

Misitu ya mvua ya tropiki ni makao ya aina nyingi ya ndege Chini kuna maelezo ya ndege wachache wa msitu wa mvua.

Kasuku ya Afrika ya rangi ya kijivu
Pied Hornbill ya Asia
Capped Lory Nyeusi
Macaw ya Rangi ya Dhahabu na Samawati
Concave-Casqued Hornbill
Double Wattled Cassowary
Fiery-Billed Aracari
Cassowary iliyo na Chingo ya rangi ya Dhahabu
Turaco Kubwa ya Samawati
Hyancinth Macaw
Kizamiadagaa
Korongo Nyeupe
Motmot
Njiwa ya Nicobar
Kasuku
Tausi
Rainbow Lorikeet
Lorikeet Nyekundu
Rhinoceros Hornbill
Kwarara Nyekundu
Macaw Nyekundu
Swainson’s Toucan
Toucan
Njiwa ya Western Crowned
Wreathed Hornbill
Cockatoo yenye Shungi ya Majano

**Reptilia na Amfibia za Msitu wa Mvua**

---

Misitu ya mvua ya tropiki ni makao ya aina nyingi ya reptilia na amfibia Chini kuna maelezo ya reptilia na amfibia wachache wa msitu wa mvua.

REPTILIA
Vijusi
Anole
Kinyonga
Crowned Adamid
Mjusi Kafiri wa Mchana
Iguana ya Fiji
Mjusi Kafiri yenye Macho ya Majani
Iguana
Kinyonga cha Matawi
Mjusi Kafiri ya Leaf-Tail
Mangrove Monitor
Mjusi wa Water Monitor
Nyoka
Chatu
Nyoka ya Panya ya Pangoni

Nyoka ya Gmelin’s Bronzeback
Kipiribao ya Majani
Chatu ya Mti ya Majani
Mamba
Mamba za Afrika
Caiman
AMFIBIA
Chura
Chura ya Blue Poison Dart
Chura ya Giant Monkey
Chura ya Green Poison Dart
Chura ya Rangi ya Dhahabu ya Panama
Chura ya Tomato
Chura ya White’s Tree
Chura ya Yellow Poison Dart

**Samaki ya msitu wa mvua**
---------------------------------------------------------------------------------

Maji ya misitu ya mvua ya tropiki – ikiwamo mito, viziwa na vinamasi – ni makao ya kiwango kikubwa ya aina ya samaki ya maji safi. Eneo ya Amazon pekee ina juu ya 3000 ya aina inayotambika na labda kiwango kama hiyo isiyojulikana.

Samaki nyingi ya maji safi ya tropiki inayowekwa kwa tangisamaki mwanzo wao ni msitu wa mvua. Samaki kama Angelfish, Neon Tetras, Discus na Kambale zinatoka msitu ya tropiki ya Amerika Kusini na Danios, Gouramis, Siamese na Fighting Fish (au Betta) na Clown Loach zinatoka Asia.

**Wadudu wa Msitu wa Mvua**
---------------------------------------------------------------------------------

Aina nyingi zaidi za wanyama wanayopatikana kwa msitu wa mvua ni wadudu. Karibu kiwango cha robo cha aina wa wanyama ambaye wamepewa jina na kuelezwa na wanasayansi ni kombamwiko. Karibu aina ya kombamwiko 500,000 zinajulikana kuishi.

WADUDU
Pepeo ya Archduke
Kombamwiko
Vipepeo
Kipepeo ya Clear-Wing
Dragonfly
Kombamwiko wa kinyesi
Pepeo ya Bundi
Jongoo ya Pill
Vunjajungu

**Watu wa Msitu wa Mvua**
---------------------------------------------------------------------------------

Misitu ya mvua ya tropiki ni makao ya watu wa makabila ambayo wanatengemea mazingira yao kwa chakula, makao na madawa. Sasa watu wachache sana wa msitu wanakaa kwa utamaduni wao; wengi wao wameng’olewa na wa setla kutoka nje au wamelazimishwa kubadili miendo ni serikali.

Kwa watu wa msitu wanayo mbaki, Amazon inatengemewa na kiwango kikubwa zaidi hata kuwa hawa watu pia wamenguzwa na dunia ya sasa. Anghalau bado wanatumia

msitu kwa kuwinda na kusanya kwa kiutamaduni, Amerindians, kama hawa watu wanaitwa, wanakuza mimea kama (ndizi, manioc na mchele) wanatumia vyombo vya magharibi kama (safuria,virai na vijiko)na wanatembeleya miji mara kwa mara kuleta chakula na vyombo kwa soko.    Lakini hawa watu wa msitu wanaweza kutufundisha mengi juu ya msitu wa mvua. Elimu yao ya miti ya dawa ya kutibu magonjwa haina mwingine na wanaelewa sana hali ya msitu wa Amazon.

Africa kuna wenyeji wa msitu wa kiasili wanaojulikana saa zingine kama vibete. Mrefu zaidi wa hawa watu ambaye anajulikana pia kama Mbuti, ni ngumu akizidi futi tano. Muundo wao mdogo unawawezesha kutembea kwa msitu kwa ufanisi mwingi kushinda watu warefu zaidi.

**USTAARABU MASHUHURI NDANI YA MSITU WA MVUA**

--------------------------------------------------------------------------------

Siku hizi wakaaji wengi wa msitu uishi kwenye makao ndogo au wanashughulika na windaji na ukusanyaji wa kuhamahama. Mbeleni misitu ya mvua ya tropiki na eneo za karibu zilitegemewa na ustaarabu kama yule wa Mayas, Incas, Aztecs ambayo iliunda jamii zinye changamano na zikasaidia sana sayansi.

Hizi ustaarabu mashuhuri zilipambana na shinda za kimazingira kama zile tunapambana nazo ( Upotezi kubwa wa msitu, upotezo wa udongo, watu wengi, ukosefu wa maji) Kwa wa Maya uharibifu wa mazingira labda ulikuwa mkubwa sana hata wakuwangusha.

**ELIMU YA MITI YA DAWA YA WATU WA KIASILI**

--------------------------------------------------------------------------------

Moja wapo wa sehemu changanifu ya utafiti wa misitu ya tropiki ni ethnobotany ambayo ni elimu ya jinsi watu wanatumia mimea asili kutibu magonjwa. Watu wa msitu wana elimu ya kushangaza ya memea ya dawa inayotibu kila kitu kutoka kuumwa na nyoka mpaka kuvu.

Kwa sasa dawa nyingi zinayotumiwa kwa nchi za magaribi zimetengenezwa na mimea na asilimia 70 ya mimiea inayotambulika na Tasisi ya Seretani ya Taifa ya Marekani kuwa na uwezo wa kuzuia seretani zinapatikana tu kwa msitu wa mvua wa tropiki.

Kwa kawaida elimu ya mimea ya dawa inafanwa na Shaman au mganga wa kijiji. Shaman anatibu wagonjwa mara nyingi wakati wa sherehe na ibada za undani akitumia mimea iliyokusanyo kutoka msitu uliozingira.

**NINI ILITENDEKA KWA WATU ASILI WA AMAZON?**

--------------------------------------------------------------------------------

Mbele ya dunia mpya kuzumbuliwa na Christopher Colombus karne ya 15 watu kadiri wa 7-10 millioni wa Amerindians (Jina ya watu asili wa Amerika) waliishi misitu ya mvua ya Amerika nusu ya hawa Brazil. Miji mikubwa ilipatikana Andes na Amazon ilitegemewa na jamii za ukulima.

Kuasiri kwa wazungu kulileta mwisho wa ustaarabu asili ya Amerika ya kati na kusini. Wazungu walibeba magonjwa ambayo iliua wa millioni wa Amerindians na ndani ya miaka 100 tango kuasiri kwa wageni hawa, namba ya watu wa Amerindian ilishuka kwa kiwango ya asilimia 90.  Wengi walionusurika waliishi ndani ya msitu: Kwa sababu ya kusukumwa huko ni Wazungu au kwa sababu ya kuishi huko kwa kimila kwa vikundi vidogo.

## WATOTO NDANI YA MSITU WA MVUA

Mbali na kusioangalia TV, kutumia mtandao au kucheza michezo ya video, watoto wa msitu wa mvua wanafanya mambo mengi ambapo labda unafanya. Wanacheza na marafiki, wanasaidia jamii zao na kazi na wanaenda shule.

Kwa sababu watoto wa msitu wa mvua wanaishi karibu na dhati kuliko mtoto wa Marekani wa kawaida wanasoma mamba ambayo inayowasaidia kwa mazingira yao. Kutoka miaka midogo watoto wengi wanajua kutega samaki, kuwinda na kukusanya vitu na chakula kutoka msitu. Badala ya kuenda kwa kiwanja ya michezo au kwa maduka kwa burudani, watoto wa mahali kama Amazon wanatumia masaa yao mengi nje wakicheza msituni na kwa mito.

## MISITU YA MVUA NI MUHIMU KWA NINI?

Misitu ya mvua ni muhimu kwa mifumo ya mazingira ya ulimwengu. Misitu ya Mvua:
+ Ni makao ya memea na wanyama wengi;
+ inasaidia kuimarisha hewa ya dunia;
+ inalinda kutoka mafuriko, ukame na uteremeko ya undogo;
+ ni chanzo ya madawa na chakula;
+ inategemewa na watu wamakabila; na
+ inavutia kutembeleya

## MISITU YA MVUA INASAIDIA KUIMARISHA HEWA

Misitu ya mvua inasaidia kuimarisha hewa ya ulimwengu kwa kunywa dioksidi ya kaboni. Dioksidi ya kaboni ya kupita kiasi inaaminiwa kuchangisha kwa ubadilishaji wa hewa kwa kuongeza joto duniani. Basi misitu ya mvua ni muhimu kwa kukabili ongezeko ya joto duniani.

Misitu pia inaathiri hali ya hewa ya eneo kwa kutengeneza mvua na kupoesha joto.

## MISITU YA MVUA NI MAKAO YA MEMEA NA WANYAMA

Misitu ya mvua ni makao ya aina nyingi ya memea na wanyama wa dunia ikiwamo viumbo venye hatarini.  Vile misitu inakatwa viumbo mingi inapotea. Viumbo vingine vya msitu wa mvua zinaweza tuu kuishi kwa mazingira yao ya kiasili. Zoo haziwezi kuokowa wanyama wote.

## MISITU YA MVUA INASAIDIA KUIFADHI MUHULA WA MAJI

Misitu ya mvua inasaidia kuifadhi muhula wa maji. Kulingana na Marekani Uchunguzi wa Jiografia, “muhula wa maji inayojulikana pia kama muhula wa hydrologic, inaeleza mwendo unayoendelea wa maji juu, chini, na kwa sakafu ya ardhi.”

Kazi ya misitu ya mvua kwa muhula wa maji ni kuongeza maji angani kupitia njia ya kutoa mvuke (ambapo wanatoa maji kutoka majani yao wakati wa usanidinuru). Hii mvuke inachangia kwa kuunda mawingo ya mvua inayorejesha maji kwa msitu wa mvua. Amazon, asilimia 50-80 ya mvuke inabaki kwa mfumo wa mazingira wa muhula ya maji.

Miti ikikatwa mvuke unaponguka kwa angani na mvua inapungua na saa zingine inaleta ukame.

**MISITU YA MVUA INAPUNGUZA UTEREMEKO WA UNDOGO**

---

Mizizi ya miti ya msitu wa mvua na memea inasaidia kutenga undogo. Miti ikikatwa hakuna kinga ya ardhi na undogo unaoshwa haraka ni mvua. Hii njia ya kuosha undogo inaitwa uteremeko wa undogo.

Vile undogo inaoshwa kwa mito inaleta shida kwa samaki na watu. Samaki zinaumia kwa sababu maji inachafuka na watu wanakuwa na tabu ya kuongoza chombo majini kwa sababu urefu wake unapungua kwa sababu ya ongezeko ya uchafu majini. Vilevile wakulima wanapoteza undogo wa juu ambayo ni muhimu kwa kukuza memea.

**MISITU YA MVUA INAHARIBIWA KWA NINI?**

---

Kila mwaka eneo ya msitu wa mvua inayolingana na New Jersey inakatwa na kuharibiwa.  Memea na wanyama walioishi kwa hiyo misitu wanakufa au lazma wapate msitu mpya wa kuita nyumbani. Misitu ya mvua inaharibiwa kwa nini?

Binadamu ni chanzo kubwa ya uharibifu wa msitu ya mvua na upunguzi wa misito.
Binadamu wanakata misitu ya mvua kwa sababu nyingi, ikiwamo:
+ miti ya mbao na miti ya kuni;
+ ukulima wa shamba ndogo na kubwa;
+ ardhi kwa wakulima maskini ambayo wana mahali nyingine ya kuishi;
+ mahali ya kulisha ngombe; na
+ utengezaji wa barabara

**KUKATA NA KUKUSANYA MITI KWA MSITU WA MVUA**

---

Sababu moja ya uharibifu wa msitu wa maji ni ukataji wa miti. Aina nyingi ya mbao ya samani, sakafu na ujenzi inavunwo kutoka misitu ya tropiki ya Afrika, Asia na Amerika Kusini. Kwa kununua aina zingine ya vyombo ya mbao mahali kama Marekani inachangia kwa uharibifu wa misitu ya mvua.

Ingawaje kukata miti inaweza kuendelea na utaratibu ambayo inapunguza uharibifu wa mazingira, kukuta miti kwingi ndani ya msitu wa mvua unafanwo kwa uharibifu sana. Miti kubwa inakatwa na kuburutwa msituni na barabara zinafungulia wakulima maskini eneo mbali ya msitu kwa ukulima. Africa wakatamiti wanategemea nyama ya msitu kwa protini.  Wanawinda wanyama kama sokwe, swala na sokwe mtu kwa chakula.

Utafiti unaonyesha kwamba aina ya wanyama inayopatikana kwa msitu unaokatwa miti na chini ya nambari inayopatikana kwa msitu usioguzwa. Wanyama wengi wa msitu wa mvua hawawezi kuishi kwa mazingira hii imeyobadilika.

Wenyeji mara mingi wanategemea uvuno wa miti ya msitu wa mvua kwa kuni na vifaa ya ujenzi.  Mbeleni matendo kama haya haikukuwa hatari sana kwa mfumo wa mazingira.  Lakini sasa kwa eneo ambazo zina ummati kubwa wa watu, watu wale wanaokota miti kutoka eneo ya msitu ya mvua wanaweza kuleta uharibifu mkubwa Kwa mfano misitu inayopakana na kambi ya wakimbiaji katikati ya Afrika (Rwanda na Congo) ziming’olewa karibu miti yote kwa eneo zingine.

**UKULIMA NDANI YA MSITU WA MVUA**

--------------------------------------------------------------------------------

Kila mwaka maelfu ya maili ya msitu wa mvua inaharibiwa kwa nia ya ukulima. Vikundi viwili ambayo inachangilia kubadili msitu wa mvua kuwa shamba ni wakulima maskini na mashirika.

Wakulima maskini mahali mingi ya dunia wanategemea kukata miti kulisha jamii zao. Bila njia ya kupata ardhi bora zaidi ya ukulima hawa watu wanatumia kukata na kuchoma kung'oa vipande ya msitu kwa muda mfupi. Kawaida wanalima ardhi walichokoa kwa miaka kadhaa kabla ya unono wa ardhi kuisha na kuwalazimisha kuhama kwengine.

Mashirika ya ukulima yana ondoa msitu wa mvua kuliko zamani, sana sana Amazon ambapo akari kubwa ya msitu wa mvua inabadilishwa kuwa mashamba ya maharagwe ya soya. Wataalamu wengine wanaamini kuwa siku moja Amerika kusini itakuwa na mashamba kama yale ya katikati magharibi ya Marekani. Mengi ya mashamba haya kubwa intatoka kwa msitu wa mvua wa Amazon.

**NGOMBE NDANI YA MSITU WA MVUA**

--------------------------------------------------------------------------------

Kukati miti kwa sababu ya shamba za kulisha ngombe ni sababu kubwa ya uharibifu wa msitu wa Amazon na Brazil sasa inatoa nyama nyingi kushinda hapo awali. Mbali na kulisha ngombe kwa chakula wamiliki ardhi wengi wanatumia ngombe kuongeza shamba zao. Kwa kuweka ngombe zao tu kwa sehemu yam situ, wamiliki ardhi wanaweza kupata haki ya umiliki wa ardhi.

**UJENGAJI BARABARA NDANI YA MSITU WA MVUA**

--------------------------------------------------------------------------------

Ujengaji njia na barabara ndani ya msitu wa mvua ufungulia sehemu kubwa kwa maendeleo. Barabara ya Trans-Amazonia, Brazil ilichangia kwa uharibifu wa eneo kubwa ya msitu ni wakoloni maskini, wakata miti na wabahatishaji wa ardhi. Africa barabara za kukata miti zinapeya nafasi jangili ambao wanawinda wanyama waliko hatarini kwa sababu ya nyama ya kichaka wanayouziya wakaaji wa miji.

**CHANGIYO YA UMASKINI KWA UHARIBIFU WA MSITU**

--------------------------------------------------------------------------------

Umaskini unachangia sana uharibifu wa misitu. Misitu ya mvua ya dunia inapatikana kwa eneo maskini zaidi ya ulimwengu. Watu wanao kaa ndani na karibu na misitu ya mvua wanategemea mifumo ya mazingira kwa maisha yao. Wanakusanya matunda na mbao na wanawinda wanyama kwa kuweka nyama mezani na wanalipwa na mashirika kusanya rasilimali kutoka sehemu ya msitu.

Watu wengi maskini wa mashambani njia zile sisi wa nchi za magharibi wana chukuwa kama kawaida. Hawa watu ni ngumu wakipata nafasi ya kuenda chuo au kuwa daktari, mfanyi kazi wa kiwanda au katibu. Lazima waishi kutoka ardhi inayowazunguka na watumie rasilimali yoyote wanaopata. Umaskini wao ni gharama kwa dunia nzima kutokana na hasara ya misitu ya mvua na wanyama. Mbila kujaliya hawa watu misitu ya mvua haiwezi kuokolewa.

**TUNAWEZA KUOKOA MISITU YA MVUA AJE?**

--------------------------------------------------------------------------------

Misitu ya mvua inaisha haraka sana. Habari njema ni kwamba kuna watu wengi wanataka kuokoa misitu ya mvua. Habari ngumu ni kwamba kuokoa misitu ya mvua

itakuwa rahisi. Itachukua bidii ya watu wengi wakifanya kazi pamoja kuhakikisha misitu ya mvua na wanyama wao itakuwa kwa watoto wako kufurahiya na kushukuru.

Njia zingine za kuokoa misitu ya mvua na kwa kiwango kubwa mifumo ya mazingira duniani ni tia maanane kwa "MITI"
+ Semesha wengine juu ya umuhimu wa mazingira na vile wanaweza kusaidia kuifadhi misitu ya mvua.
+ Rejesha mifumo ya mazingira iloyo haribiwa kwa kupanda miti kwa ardhi ambapo misitu imekatwa.
+ Himiza watu wakae kwa njia ambayo haihasiri mazingira
+ Anzisha mbuga zaa kulinda misitu ya mvua na wanyama
+ Unga mkono mashirika inayotenda mambo kwa njia ambayo inapunguza uharibifu wa mazingira.

**KUOKOA MISITU YA MVUA NA ELIMU**

--------------------------------------------------------------------------------

Elimu ni sehemu muhimu ya kuifadhi misitu ya mvua ya ulimwengu. Watu lazima waone urembo na waelewe umuhimu wa hii misitu ndivyo watake kuilinda. Elimu ya mazingira inatakiwa nchi za magharibi kama Marekani na nchi zilizo na msitu wa mvua kama Bolivia na Madagascar.

Marekani, watu wanatakiwa waelewe mchangio wao kwa upotefu wa misitu ya mvua. Kwa mfano kununua vyombo vingine kama mahogany zinachangia kwa kukata miti ya misitu ya mvua nchi zingine. Wamarekani wakijitahidhi kuelewa mambo ya mazingira tunaweza kuelewa ile tunapoteza msitu wa mvua ukipoteya. Tunaweza kuamua kununua vifaa na kuunga mkono mashirika na vikundi zinayosaidia msitu wa mvua.

Kwa nchi za msitu wa mvua watu saa zingine waelewi umuhimu wa misitu. Kwa njia ya mipango ya elimu hawa watu wanaweza kujua kwamba misitu zinapeyana huduma muhimu kama (maji safi) na ni makao ya memea na wanyama isiyopatikana mahali pengine duniani.  Watoto wachache mahali kama Madagascar wanafahamu kwamba Lemurs zipatikani Marekani. Unafurahi ukielewa kwamba Lemurs zinaishi Madagascar pekee.

**KARABATI NA REJESHA MISITU YA MVUA**

--------------------------------------------------------------------------------

Tukijaribu kuifadhi misitu ya mvua tunahitaji kuangalia vile misitu iliyoharibiwa inaweza kurejeshwa kwa afya. Hata kama kurejesha msitu wa mvua haiwezekani misitu ya mvua yaweza kurudi baada ya kukatwa –- sana sana kama inausaidizi wa kupanda miti.  Saa zingine inawezekana kutumia ardhi iliyokatwa miti kwa ukulima bora ndiye iweze kupeya watu wa karibu chakula. Hawa watu wakiwa na chakula watahitaji kukata msitu tena kupanda mimea.

Eneo moja yenye mafanukio inaangalia jamii za zamani za msitu wa Amazon kabla ya kuasiri kwa wazungu karne ya 15.   Inaonekana hawa watu waliweza imarisha undogo wa msitu wa mvua, ambaye haikuwangi nuno sana kwa kutumia makaa na mafupa ya wanyama.  Kwa kuongeza ubora wa ardhi eneo kubwa ya Amazon ambaye imekatwa miti inaweza kutumiwa kwa ukulima.  Hii inaweza kupunguza mkazo wa ardhi kwa eneo yam situ wa mvua kwa mambo ya ukulima.    Pia undogo wa "terra preta" kama inaitwa inaweza kutumiwa kusaidia kupambana na ongezeko ya joto duniani kwa sababu inakunywa dioksidi ya kaboni, gasi muhimu ya greenhouse.

**HIMIZA WATU WAKAE KWA NJIA AMBAYE HAIHASIRI MAZINGIRA**

--------------------------------------------------------------------------------

Sehemu moja muhimu ya kuifadhi misitu ya mvua na mazingira ni kuhimiza watu wote wakae kwa njia ambazo zina hasiri dunia yao kidogo. Kuendesha gari fanisi, kuifadha maji, kuzima taa usiyotumia na kurejesha vyomba ni njia ambaye jamii yako inaweza kupunguza athari yenu kwa mazingira.

Nawezakufanya nini kusaidia mazingira?

Kwa nchi ya msitu wa mvua wasayansi wengi na mashirika zinafanya kazi kusaidia wenyeji waishi kwa njia zinazo punguza uharibifu wa mazingira.  Watu wengine wanaita hii "maendeleo ya kudumisha"  Maendeleo ya kudumisha inalengo ya kuboresha maisha ya watu na pia kuifadhi mazingira.  Bila kuboresha maisha ya watu waokaa ndani na karibu ya misitu ya mvua itakuwa ngumu sana kuifadhi mbuga na wanyama. Kuifadhi mazingira lazima iwe ya mafanukiyo kwa wenyenji ndivyo mbuga zifaulu.

**ANZISHA MBUGA ZAA KULINDA MISITU YA MVUA NA WANYAMA**

---

Kuunda eneo zimeyolindwa kama mbuga za taifa ni njia nzuri ya kuifadhi misitu ya mvua na mifumu nyengine ya mazingira. Eneo zimeyolindwa ni sehemu ambaye zinapewa ulinzi kwa sababu ya umuhimu wa mazingira au utamaduni wao. Kwa jumla eneo zimeyolindwa zinasimamiwa na serikali na inatumiwa ulinzi wa askari wa msitu kuhakikisha sheria za mbuga na kulinda kutoka mambo ya uhalifu kama kuwinda na kukata miti.

Mbuga za sasa zinalinda nyingi ya viumbo vya dunia ambayo iko hatarini. Wanyama kama Panda wanapatikana tu eneo zimeyolindwa.

Mbuga zinafanikiwa zaidi kama zinaugwo mkono na wanyeji waoishi karibu na eneo imeyolindwa. Wenyeji wakishugulika na mbuga wanaweza kuunda "Ulinzi wa jamii" kulinda mbuga kutoka kwa kukatwa miti na ujangili.

Njia mwafaka ya kuifadhi misitu ya mvua ni kuhuzisha wenyeji kwa usimamizi wa mbuga.  Wenyeji wanaelewa zaidi juu ya msitu kuliko watu wengine na wanamanufaa ya kuifadhi mfumo wa mazingira yenye rutuba inayowapatia chakula, makao na maji safi.   Utafiti umegundua kwa kesi zengine "vijiji vya wenyenji" zinaweza kuifadhi msitu wa mvua vyema kushinda "mbuga ya taifa" Amazon.

Mbuga pia zinaweza kusaidia uchumi wa nchi za msitu wa mua kwa kuvutia watalii ambayo wanalipa ada ya kuingia na wanaajiri waongozi wa porini na wananunua vyombo kama vikapu, shati na bangili zilizo na makete.

**UNGA MKONO MASHIRIKA AMBAYE HAIHARIBU MAZINGIRA**

---

Siku hizi kuna kampuni nyingi zinahisika na mazingira. Hizi kampuni zinatafuta njia za kupunguza athari yao kwa duniani inayowazunguka kwa kutumia bidhaa mara nyingi, kupunguza utumizi wa kawi na ku unga mkono juhudi za nchi zingine. Wateja kama wewe na wazazi wako wana saidia kampuni hizi kwa kununua bidhaa na huduma zao mazingira itafaidika.

Namna ya kujua kama kampuni haiathiri mazingira

**UTALII WA MAZINGIRA**

---

Utalii wa mazingira ni njia ya kutembea yenye wajibu inayofurahiya mazingira na mila. Utalii wa mazingira inatakiwa isiathiri mazingira sana na ichangie kwa maslahi ya wakaaji.

## UNAWEZA KUFANYA NINI NYUMBANI KUSAIDIA MAZINGIRA

Kuna vitu kadhaa unaweza kufanya nyumbani kusaidia kupunguza uathiri wako kwa mazingira.

+ Zima taa usiyohitaji. Balbu ikichomeka badilisha na balbu zinayohifadhi kawi
+ Usipoteze maji.
+ Tumia vitu tena.
+ Himiza wazazi wako wapeleke gari zisiyo kunywa mafuta mengi na wasiweke nyumba joto kuliko kiasi.
+ Usiwashiliye wanyama wako waende kama hauwataki tena. Mbele ya kununua mnyama wa nyumbani hakikisha utaituza. Kuwa na mnyama wa nyumbani ni wajibu.

Mambo unaweza fanya kusaidia kuifadhi misitu ya mvua:

+ Usinunue bidhaa ziliyotengezwa na nguzi za wanyama wa pori
+ Usinunue wanyama wa kigeni wameokotwa porini. Unaweza kuuliza duka za wanyama wa nyumbani kama wanyama walichikwa porini au walilewa. Wanyama wa kulewa hawathiri mazingira sana

Nunua karatasi imeyotengezwa na mabaki au marudio.

+ Usinunue vifaa vya mbao kutoka Indonesia, Malaysia, Brazil au Afrika mbali tu ujue zimetoka kwa mgawaji anayotuza mazingira. Njia nzuri ya kujua kama mbao ni haiathiri msitu wa mvua ni kama ina cheti ya kuhakikisha. Mfano ni cheti ya FSC ambaye inamaanisha mbao inatoka kwa misitu inayosimamiwa kwa njia nzuri.
+ Soma juu ya misitu ya mvua na memea na wanyama wanayo kaa ndani yake. Ambiya marafiki na wazazi umuhimu wa misitu ya mvua.

## SHERIA

Ruhusa ya kutumia nyaraka hii kwa kupeyana bure kupitiya maandishi na njia nyengine imepewanywa, ile tuu mongabay.com ipewe sifa ya mwanzishi.

Mongabay.com inalenga kuinua uvutio wa wanyama na mbuga zao ikijulisha juu ya mambo ya mazingira. Kama haijatajwa mambo yote kwa hii tovuti imeandikwa na Rhett Butler.